# OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

## KALENDA YA MATUKIO YANAYOHUSU UTEKELEZAJI WA SHERIA YA VYAMA VYA SIASA SURA YA 258 NA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI SURA YA 278

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| **SHERIA YA VYAMA VYA SIASA** | | | | | |
| 1. | Mara baada ya kupata usajili wa kudumu | Chama cha siasa kinapaswa kuwa na akaunti ya benki ambayo kitaweka mapato na matumizi ya fedha zake. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa | |
| 2. | Mara baada ya kupata sifa ya kupata ruzuku kutoka Serikalini | Chama cha siasa kinapaswa kuwa na akaunti ya benki maalumu ambayo kitaweka mapato na matumizi ya fedha za ruzuku pekee. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa | |
| 3. | Muda wote wa uhai wa chama | Chama cha siasa kinapaswa kutunza na kuhuisha rejista zifuatazo:<br><br>1. Rejista ya wanachama wake.<br><br>2. Rejista ya viongozi wa chama katika kila ngazi ya utawala ya chama.<br><br>3. Rejista ya wajumbe wa vikao vya chama katika kila ngazi za utawala wa chama | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 8C(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa.<br><br>Kanuni ya 15(1)(2) na (4) ya Kanuni za Usajili na Ufuatilaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| 4. | Ndani ya muda ambao Msajili ataelekeza | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa au nyaraka yoyote ya chama inayohusu utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa. | Katibu Mkuu au kiongozi husika wa chama | Kifungu cha 5B cha Sheria ya Vyama vya Siasa, 1992 | |
| 5. | Ndani ya siku 30 baada ya chama kupata usajili wa kudumu | Chama cha siasa baada ya kupata usajili wa kudumu, kitatakiwa kuwasilisha kwa Msajili wa vyama vya siasa, kiapo cha maandishi kikieleza mali zake, matumizi yake, michango, misaada ya kifedha na isiyokuwa ya kifedha kilichopata na kutumia tangu kianzishwe. | Katibu Mkuu | Kifungu cha 12C(1) Cha Sheria ya Vyama vya Siasa, 1992. | |
| 6. | Siyo zaidi ya miaka mitano tangu kufanyika kwa uchaguzi mkuu wa viongozi wa chama. | Chama cha siasa kinapaswa kuandaa mkutano mkuu na kuchaguzi viongozi wa kitaifa | Mwenyekiti wa Taifa na Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 16(2)(3) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | |
| 7. | Siyo zaidi ya siku ishirini na nane kabla ya tarehe ya kufanya mkutano mkuu | Chama cha Siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya nia ya kufanya mkutano mkuu, kikieleza tarehe ya kufanyika mkutano huo, muda, jina la ukumbi, wilaya na mkoa mkutano utakapofanyika. | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 17 ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| 8. | Siyo zaidi ya siku sitini (60) tangu chama kipate usajili wa kudumu | Kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa majina na anuani za wajumbe wa bodi ya wadhamini na cheti cha usajili wa bodi hiyo. | Katibu Mkuu | Kifungu cha 21(2)(a)(b) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, 1992 | |
| 9. | Kabla ya mwaka mpya wa fedha wa chama kuanza. | Chama cha siasa kinapaswa kuandaa bajeti ya chama kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha wa chama. | Mwenyekiti wa Taifa na Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 5(c) ya Kanuni za kuandaa taarifa za fedha za vyama vya siasa "Political Parties (Financial Accounting) Regulations, 2019 | |
| 10. | Mwezi Januari kila mwaka | Chama cha Siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa zifuatazo:-<br><br>"(i) revenue and ex penditure report;<br>(ii) cash flow state- ments; and<br>(iii) budget implementation report." | Mwenyekiti wa Taifa na Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 5(e) ya Kanuni za kuandaa taarifa za fedha za vyama vya siasa | |
| 11. | Kabla ya tarehe 30 Juni kila mwaka | Chama cha Siasa kinapaswa kuandaa na kuidhinisha bajeti yake ya mapato na matumizi kwa ajili yam waka ujao wa fedha | Kamati tendaji na Halmashauri Kuu ya chama | Kanuni ya 5(c) ya Kanuni za kuandaa taarifa za fedha za vyama vya siasa | |
| 12. | 30 Juni ya kila mwaka | Baada ya mwisho wa Mwaka wa fedha wa kila chama cha siasa, chama kinapaswa | Katibu Mkuu | Kifungu cha 18A(1) | |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuanza kuandaa taarifa za fedha na mali za chama kwa ajili ya kuwasilisha katika mamlaka husika. | | | |
| 13. | Sio zaidi ya tarehe 30 Septemba kila mwaka | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha taarifa za fedha za chama (financial statements) kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikal (Controller and Auditor General (CAG)) kwa ajili ya ukaguzi. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 18A(2)(a)cha Sheria ya Vyama vya siasa, 1992<br><br>Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Taafia za Fedha za Vyama vya Siasa. (the Political Parties (Financial Accounting) Regulations, 2019) | |
| 14. | Siyo zaidi ya siku sitini (60) baada ya madiliko ya wajumbe wa Bodi ya Wadhamini kusajiliwa na Mamlaka husika | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa za usajili wa mabadiliko ya mjumbe/wajumbe wa Bodi ya Wadhamini wa chama pamoja na nyaraka inayothibitisha usajili huo. | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 28(4) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | |
| 15. | Ndani ya siku 14 baada ya siku ya kufanya mabadiliko ya uongozi wa kitaifa | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya siasa taarifa ya mabadiliko ya uongozi wa kitaifa kwa kuonyesha kiongozi aliyeondoka na | Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 26(1) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 7A |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | aliyechaguliwa/teuliwa. | | | |
| 16. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kiongozi wa kitaifa wa chama kuondoka madarakani kwa njia yoyote ile. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya kuondoka madarakani kiongozi huyo. | Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama au wawakilishi wao | Kanuni ya 26(2) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 7B |
| 17. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kiongozi wa kitaifa wa chama kuteuliwa au kuchaguliwa. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya kuteuliwa au kuchaguliwa kiongozi wa husika wa kitaifa. | Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama au wawakilishi wao | Kanuni ya 26(3) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 7C |
| 18. | Angalau miezi 2 kabla ya kuwa mshirika, mwanachama au kushirikiana na taasisi yoyote ya nje ya nchi | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya nia ya kujiunga katika ushirikia huo. Taarifa hiyo inapaswa kueleza jina la taasisi husika, anuani ya simu na makazi, barua pepe ya simu taasisi hiyo, madhumuni ya ushirikiano huo na majukumu ya taasisi hiyo. | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 18(1) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji | PP. 11 |
| 19. | Siku 14 baada ya chama cha siasa kujitoa katika ushirika au ushirika kukoma. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya | Katibu mkuu wa chama | Kanuni ya 18(6) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 12 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kujitoa au kukoma kwa ushirika huo. | | | |
| 20. | Miezi mitatu kabla ya mchakato wa uchaguzi kuanza. | Vyama vya siasa vilivyosaini mkataba wa ushirikiano kabla ya uchaguzi mkuu, vinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa mkataba huo wa ushirikiano. | Katibu mkuu wa chama | Kifungu cha 11A(4) cha Sheria ya Vyama vya siasa<br><br>Kanuni ya 19 ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji. | PP. 13 |
| 21. | Ndani ya siku 14 baada ya vyama vya siasa kusaini mkataba wa ushirikiano baada ya uchaguzi mkuu. | Vyama vya siasa vilivyosaini mkataba wa ushirikiano baada ya uchaguzi mkuu, vinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa mkataba huo wa ushirikiano. | Makatibu wakuu wa vyama vilivyosaini mkataba wa kushirikiana | Kifungu cha 11A(4) cha Sheria ya Vyama vya siasa<br><br>Kanuni ya 19 ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji. | PP. 13 |
| 22. | Baada ya Ilani ya Uchaguzi kuidhinishwa na kikao husika cha chama cha siasa. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha ilani hiyo ya uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ikiwa imesainiwa na kugongwa muhuri wa chama | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 20 ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 14 |
| 23. | Siku thelathini (30) kabla ya kutoa mafunzo husika | Mtu au taasisi yoyote inayotaka kutoa mafunzo kwa vyama vya siasa, inapaswa kuwasilisha taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa. Taarifa hiyo itaambatana na cheti cha usajili, lesini ya kutoa mafunzo husika au ya aina hiyo, katiba | Mtu binafsi au Mkutugenzi Mtendaji wa taasisi inayotaka kutoka mafunzo | Kifungu cha 5A cha Sheria ya Vyama vya Siasa<br><br>Kanuni ya 21 ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 15 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ya taasisi na CV ya viongozi wa taasisi. Kwa mtu binafsi anapaswa kuambatisha, CV,vyeti vya taaluma na kitambulisho. | | | |
| 24. | Kabla ya kufanyika kikao cha chama cha siasa cha kuidhinisha katiba na/au kanuni mpya au marekebisho ya katiba na/au kanuni za chama husika. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha ombi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa la kufanya mabadiliko hayo. Ombi hilo la chama cha siasa liambatane na nakala ya katiba au kanuni mpya au marekebisho yanayopendekezwa | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 22(1)(2) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 16 |
| 25. | Kabla ya kufanyika kikao cha chama cha siasa cha kuidhinisha madiliko ya jina la chama au kifupi chake. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha ombi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa la kufanya mabadiliko hayo. Ombi hilo liambatane na jina jipya au kifupi kinachopendekezwa | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 22(1)(3) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 17 |
| 26. | Kabla ya kufanyika kikao cha chama cha siasa kuidhinisha madiliko ya kadi ya uanachama, ishara, nembo au bendera ya chama | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha ombi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ya kufanya mabadiliko hayo. Ombi liambatane na kadi, ushara, nembo au bendera mpya au marekebisho | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 22(1)(4) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 18 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | yanayopendekezwa. | | | |
| 27. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya kufanya marekebisho katika katiba au kanuni za chama cha siasa. | Chama cha Siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya marekebisho hayo ikiambatana na barua ya utambulisho, nakala ya majina ya wajumbe waliohudhuria mkutano huo na saini zao, muhtasari wa mkutano na maelezo ya ibara zilizorekebishwa. | Mwenyekiti wa Taifa na Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 24(1) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 19 |
| 28. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya kufanya mabadiliko ya jina la chama cha siasa au kifupi chake. | Chama cha Siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, taarifa ya mabadiliko hayo ikiambatana na barua ya utambulisho, nakala ya majina ya wajumbe waliohudhuria mkutano huo na saini zao, muhtasari wa mkutano na maelezo ya ibara zilizorekebishwa. | Mwenyekiti wa Taifa na Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 24(2) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 20 |
| 29. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya ambayo yamefanyika mabadiliko ya kadi ya uanachama, ishara, nembo au | Chama cha Siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya mabadiliko hayo ikiambatana na barua ya utambulisho, nakala | Mwenyekiti wa Taifa na Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 24(3) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 21 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | bendera ya chama | ya majina ya wajumbe waliohudhuria mkutano huo na saini zao, muhtasari wa mkutano na maelezo ya ibara zilizorekebishwa. | | | |
| 30. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kubadili au kufanya marekebisho katika sera au itikadi ya chama cha siasa | Chama cha Siasa kinapaswa kuwasilisha taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ya mabadiliko au marekebisho ya sera au itikadi yake ikiambatana na sera au itikadi mpya au marekebisho husika. | Mwenyekiti wa Taifa na Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 25 ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa | PP. 22 |
| 31. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mjumbe wa kikao cha chama cha siasa wa kitaifa kuondoka madarakani kwa njia yoyote ile au mwanachama kuteuliwa au kuchaguliwa kuwa mjumbe wa kikao cha kitaifa cha chama cha siasa | Chama cha Siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya mjumbe wa kikao cha chama cha kitaifa kuondoka madarakani kwa njia yoyote ile au mwanachama kuteuliwa au kuchaguliwa kuwa mjumbe wa kikao cha kitaifa cha chama | Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama au wawakilishi wao | Kanuni ya 27(1) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 23 |
| 32. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya chama cha siasa kuondoka | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya | Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama au wawakilishi wao | Kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 24 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | madarakani kwa njia yoyote ile au mwanachama kuteuliwa au kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha siasa | chama kuondoka madarakani kwa njia yoyote ile au mwanachama kuteuliwa au kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya chama hicho. | | | |
| 33. | Ndani ya siku kumi na nne (14) tangu tarehe ambayo ofisi za Makao Makuu au Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya chama zimehama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya kuhama kwa ofisi za Makao Makuu au Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya chama kutoka eneo moja kwenda lingine. | Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama au wawakilishi wao | Kanuni ya 29(1)(2) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 25 |
| 34. | Ndani ya siku kumi na nne (14) tangu tarehe ambayo sanduku la posta la ofisi za makao makuu ya chama au ofisi ndogo za makao ya chama limebadilika. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya mabadiliko ya sanduku la posta la ofisi ya makao makuu au ofisi ndogo ya makao makuu ya chama. | Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama au wawakilishi wao | Kanuni ya 29(1)(3) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 26 |
| 35. | Ndani ya siku kumi na nne (14) tangu kubadilika kwa taarifa za kiongozi wa chama cha siasa, mjumbe wa bodi ya wadhamini au mjumbe wa kikao cha chama cha siasa. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu mabadiliko hayo na kufanya kufanya mabadiliko katika rejista husika ya chama | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 30 ya Kanuni za Usajili wa Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 27 |
| 36. | Ndani ya siku kumi na nne (14) | Chama cha siasa kinapaswa | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 15 cha Sheria ya | PP. 28 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | baada ya chama cha siasa kufungua akaunti ya benki | kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya kufungua akaunti ya Benki ikionyesha:<br>1. Jina la akaunti;<br>2. Namba ya akaunti;<br>3. Jina benki na tawi ambapo akaunti imefunguliwa;<br>4. Watia saini katika akaunti hiyo; na<br>5. Madhumuni ya kufungua akaunti/matumizi ya akaunti hiyo. | | Vyama vya Siasa na Kifungu cha 11(2) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi.<br>Kanuni ya 32(1)(a) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | |
| 37. | Ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya chama cha siasa kufunga akaunti yake ya benki | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya kufunga akaunti ya Benki ikionyesha:<br>1. Jina la akaunti;<br>2. Namba ya akaunti;<br>3. Jina benki na tawi ambapo akaunti imefunguliwa;<br>4. Watia saini katika akaunti hiyo; na<br>5. Sababu ya kufunga akaunti hiyo. | Katibu Mkuu wa chama | Kanuni ya 32(1)(b) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 29 |
| 38. | Ndani ya siku 14 baada ya chama cha siasa kupokea msaada wa fedha | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha taarifa kwa Msajili wa vyama vya siasa | Katibu mkuu wa chama | Kifungu cha 13(2) cha Sheria ya Vyama Vya Siasa | PP. 30 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | au mali aina nyingine | kuhusu mapato kutoka vyanzo vifuatavyo:<br><br>1. kutoka nje ya nchi yaliyopatikana moja kwa moja au kupitia chanzo kilichopo ndani ya nchi,<br><br>2. kutoka mashirika ya kimataifa yaliyopo ndani ya nchi.<br><br>3. kutoka kwa mtu yeyote ambaye ni mkazi hapa nchini lakini sio raia.<br><br>Taarifa ieleze chanzo cha fedha hizo, namba namba ya simu, anuani ya posta na makazi ya mfadhili | | Kanuni ya 34(1) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji za Mwaka 2019 | |
| 39. | Kila baada ya miezi 3 | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa za rasilimali fedha na rasilimali nyingine ambazo, siyo fedha zinazotoka vyanzo vya ndani ya nchi, ambazo thamani yake ni zaidi ya shilingi elfu hamsini. Taarifa ieleze chanzo cha fedha hizo, namba namba ya simu, anuani ya posta na makazi ya mfadhili | Katibu mkuu wa chama | Kifungu cha 13(2)(d) cha Sheria ya vyama vya siasa ya Mwaka 1992<br><br>Kanuni ya 35 ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji za Mwaka 2019 | PP. 31 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| 40. | Mwezi mmoja baada ya kupokea ripoti ya ukaguzi wa taarifa za fedha za chama kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ripoti wa taarifa za fedha za chama iliyotoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu 18A(2)(b) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, 1992<br><br>Kanuni ya 36(1)(2) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 | PP. 32 |
| 41. | Siyo zaidi ya tarehe 30 Septemba ya kila mwaka | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa tamko la mali za chama la mwaka wa fedha uliopita likiambatana na nakala ya rejista za mali za chama hicho. | Katibu mkuu | Kifungu 14(1)(b)(ii) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, 1992<br><br>Kanuni 37(1) ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji za Mwaka 2019 | PP. 33 |
| **SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI SURA YA 278** | | | | | |
| 42. | Ndani ya siku tisini (90) kabla ya uchaguzi mkuu na wakati wote wa uchaguzi huo. | Chama cha siasa hakipaswi kupokea msaada wa aina yoyote kutoka nje ya nchi kwa ajili ya gharama za uchaguzi. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 12(1)(2)(3)(a) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi | |
| 43. | Ndani ya siku thelathini (30) kabla ya uchaguzi mdogo na wakati wote wa uchaguzi huo. | Chama cha siasa hakipaswi kupokea msaada wa aina yoyote kutoka nje ya nchi kwa ajili ya gharama za uchaguzi. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 12(1)(2)(3)(b) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi | |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| 44. | Kabla ya mchakato wa uchaguzi kuanza | Chama cha Siasa kinapaswa kuwa na akaunti ya benki maalum kwa ajili ya mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 11(2) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi | |
| 45. | Katika muda ambao Msajili wa Vyama vya Siasa ataelekeza | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi. | Kiongozi wa chama au mgombea husika. | Kifungu cha 6 cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi | |
| 46. | Ndani ya siku 7 baada ya uteuzi wa wagombea kufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Mgombea anapaswa kujaza na kuwasilisha katika mamlaka husika fomu ya tamko la gharama za uchaguzi akieleza fedha alizonazo na anazotegemea kupata ambazo atatumia kama gharama za uchaguzi katika uchaguzi husika. | Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mgombea ubunge na mgombea udiwani. | Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi<br><br>Kanuni ya 7(2)(3) ya Kanuni za gharama za Uchaguzi. | EE. 1 |
| 47. | Ndani ya siku 7 baada ya siku ya uteuzi wa wagombea kufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Kiongozi husika wa chama cha siasa anapaswa kujaza fomu EE. 2 kuthibitisha kuwa mgombea amejaza fomu EE. 1 kikamilifu. | Katibu wa chama cha siasa wa wilaya na Katibu Mkuu wa chama husika. | Kanuni ya 9(1) ya Kanuni za gharama za Uchaguzi. | EE. 2 |
| 48. | Ndani ya siku 7 baada ya uteuzi wa wagombea kufanywa na | Afisa mteule anapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama | Afisa mteule na mgombea mwenyewe | Kanuni ya 9(1)(2) ya Kanuni za gharama za Uchaguzi. | |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | vya Siasa fomu EE. 1 za wagombea zilizowasilishwa kwa Katibu wa chama zikiambatana na fomu EE. 2 | | | |
| 49. | Ndani ya siku 30 baada ya uteuzi wa wagombea kufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Chama cha siasa kitanachoshiriki uchaguzi kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa fomu EE. 3 kikieleza kiasi cha fedha kinachotarajia kutumia kama gharama za uchaguzi na kiasi cha fedha kinachotarajia kuwapa wagombea wake kama gharama za uchaguzi. | Mwenyekiti wa Bodi ya wadhamini ya Chama. | Kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Gharama za uchaguzi ,<br><br>Kanuni ya 8(1)(2) ya kanuni za gharama za uchaguzi. | EE. 3 |
| 50. | Ndani ya siku thelathini (30) baada ya siku ya uteuzi wa wagombea kufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. | Chama cha siasa kinapaswa kumtaarifu Msajili wa Vyama vya Siasa kiasi cha fedha ambacho kinatajia kuwapatia wagombea wake watumie kama gharama za uchaguzi. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 9(2)(b) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi.<br><br>Kanuni ya 8(3) ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi | EE. 4 |
| 51. | Mara baada ya kupokea zawadi, msaada, mkopo au amana ya fedha aina yoyote kwa ajili ya gharama za uchaguzi | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu zawadi, msaada, mkopo au amana ya fedha aina yoyote | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 11(2) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi<br><br>Kanuni ya 9(3) ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi | EE. 5 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kilichopokea kwa ajili ya gharama za uchaguzi. | | | |
| 52. | | Taasisi ya kiraia inayotaka kushiriki katika uchaguzi kwa kufanya uhamasishaji au tutoa elimu ya uraia inapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ikieleza fedha inayotajia kutumi kwa uhamasishaji na kutoa elimu hiyo. Taarifa iambatane na mpango kazi wa kazi hiyo. | Mtendaji Mkuu wa taasisi husika | Kanuni ya 9(4) ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi | EE. 6 |
| 53. | Mara baada ya kupokea msaada kwa ajili ya kutumia kama gharama za uchaguzi | Mgombea anapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya msaada aliopata kwa ajili ya gharama za uchaguzi. | Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mgombea ubunge na mgombea udiwani wa Tanzania Bara | Kifungu cha 11(4) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi<br><br>Kanuni ya 10 ya Kanuni za gharama za uchaguzi. | EE. 7 |
| 54. | Ndani ya siku 30 baada ya chama cha siasa kupokea msaada wa gharama za uchaguzi unaozidi shilingi milioni moja kutoka kwa mtu binafsi au zaidi ya shilingi milioni mbili | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya kupokea msaada huo ikieleza jina la mfadhili na mfadhiliwa na anuani zao za makazi, tarehe na | Bodi ya wadhamini ya Chama | Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Gharama za uchaguzi.<br><br>Kanuni ya 10 ya Kanuni za gharama za uchaguzi. | EE. 8 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | kutoka kwa taasisi. | madhumuni ya kutolewa msaada. | | | |
| 55. | Mara baada ya chama cha siasa kufanya matumizi ya gharama za uchaguzi zaidi ya kiwango kilichowekwa na sheria | Chama cha Siasa kinapaswa kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu fedha kilizotumia kama gharama za uchaguzi ambazo zinazidi kiwango kilichowekwa na sheria. Aidha, chama cha siasa hapaswi kuzidisha kiwango cha gharama za uchaguzi zaidi ya asilimia kumi na tano (15) ya kiwango kilichowekwa na sheria. | Katibu Mkuu wa chama | Kifungu cha 10(2) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi<br><br>Kifungu cha 11(a) cha Kanuni za Gharama za Uchaguzi<br><br>Kanuni ya 3 ya Kanuni za ukomo wa gharama za uchaguzi "Election Expenses (Maximum amount of funds) Order, 2010" | EE. 9 |
| 56. | Mara baada ya mgombea kufanya matumizi ya gharama za uchaguzi zaidi ya kiwango kilichowekwa na sheria | Mgombea anapaswa kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu fedha alizotumia kama gharama za uchaguzi ambazo zinazidi kiwango kilichowekwa na sheria. Aidha, mgombea hapaswi kuzidisha kiwango cha gharama za uchaguzi zaidi ya asilimia kumi na tano (15) ya kiwango kilichowekwa na sheria. | Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mgombea ubunge na mgombea udiwani wa Tanzania Bara | Kifungu cha 10(2) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi<br><br>Kifungu cha 11(b) cha Kanuni za Gharama za Uchaguzi.<br><br>Kanuni ya 3 ya Kanuni za ukomo wa gharama za uchaguzi "Election Expenses(Maximum amount of funds) Order, 2010" | EE. 10 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| 57. | Ndani ya siku 30 baada ya siku ya uchaguzi | Chama cha siasa kinapaswa kumjulisha kila mgombea wake kiasi cha fedha alichopewa kama gharama za uchaguzi. | Katibu mkuu wa chama | Kifungu cha 17(1)(b) Cha sheria ya Gharama za uchaguzi. | |
| 58. | Ndani ya siku 60 baada ya siku ya uchaguzi | Kila mgombea anapaswa kuandaa na kuwasilisha ripoti ya matumizi ya gharama za uchaguzi kwa chama chake kilichomdhamini kuwa mgombea. Mgombea urais atawasilisha kwa Katibu Mkuu wa chama, Mgombea ubunga na udiwani watawasilisha kwa mwanachama anayetekeleza majukumu ya katibu wa wilaya wa chama. | Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mgombea ubunge na mgombea udiwani wa Tanzania Bara | Kifungu cha 18(1) cha Sheria ya gharama za uchaguzi.<br><br>Kanuni ya 15(1)(2)(3)(4) ya kanuni za gharama za uchaguzi. | EE. 11 |
| 59. | Ndani ya siku 180 baada ya tarehe ya mwisho ya wagombea kuwasilisha taarifa ya matumizi ya gharama za uchaguzi kwa chama chake. | Chama cha siasa kinapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ripoti ya mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi za wagombea wake wote na chama chenyewe. | Bodi ya Wadhamini ya chama | Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya gharama za uchaguzi.<br><br>Kanuni ya 15(6) ya kanuni za gharama za uchaguzi. | EE. 12 |
| 60. | Ndani ya siku tisini (90) baada ya siku ya uchaguzi. | Taasisi ya kiraia iliyoshiriki uchaguzi kwa kufanya uhamasishaji au | Mkurugenzi mtendaji wa taasisi husika | Kifungu cha 13(4) cha Gharama za Uchaguzi. | EE. 13 |

| Na. | Tarehe | Tukio | Muhusika | Kifungu | Fomu Husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kutoa elimu inapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa kuhusu fedha ilizopokea na kutumia katika kazi hizo. | | Kanuni ya 15(7) ya kanuni za gharama za uchaguzi. | |